

MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA



Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

KANDA YA MAGHARIBI

JARIDA LA MTANDAONI JULAI 2021 – JUNI 2022





DIRA

Kuwa Mamlaka inayoongoza katika kudhibiti ubora, usalama, na ufanisi wa dawa, Vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine za afya kwa wote.



DHIMA

Kulinda afya ya jamii kwa kuzuia athari zinazoweza kujitokeza kutohana na matumizi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi.



FALSAFA

Kutoa huduma bora za udhibiti katika kulinda afya ya jamii na mazingira kwa kutumia wafanyakazi wenyewe ujuzi na ari ya kazi.



MAADILI YA MSINGI

- Uaminifu
- Kumjali mteja
- Ubora
- Kufanya kazi kwa ushirikiano
- Uwajibikaji
- Uwazi

YALIYOMO

Neno la Meneja wa Kanda	04
Ukaguzi wa maeneo yanayojihusisha na bidhaa	05
Udhibiti wa uingizaji na utoaji wa bidhaa	07
Ufuatiliaji wa madhara yatokanayo na matumizi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi	08
Elimu kwa Umma	09
TMDA kushiriki kongamano la kimataifa.	13
Marufuku ya matumizi ya bidhaa za tumbaku	14
Uteketezaji wa bidhaa	15
Utoaji huduma kwa jamii	15

BODI YA WAHARIRI

Mhariri Mkuu:

Bw. Christopher O. Migoha

Wahariri Wasaidizi:

Fredrick Luyangi
Kiboko Magigi
Evelyne Makoye

Sekretarieti:

Tumaini Petro
Ferdinand Rugambwa
Neema Minja
Juliana Kasembe
Nassib Mlangali
Daniel Johnson

NENO LA MENEJA WA KANDA YA MAGHARIBI

Nichukue fursa hii kukukaribisha kusoma jarida hili la mtandaoni juu ya utendaji kazi wa Ofisi ya TMDA Kanda ya Magharibi kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Juni, 2022, Ofisi ya TMDA Kanda Magharibi ni miongoni mwa Ofisi nane (8) za Kanda za TMDA inapatikana katika jengo la NSSF Mtaa wa Jamhuri Manispaa ya Tabora ambayo inahudumia Mikoa mitatu (3) ya Tabora, Kigoma na Katavi ikiwa na jumla ya Halmashauri 21.

Katika kipindi hiki cha kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022, Ofisi ya Kanda ya Magharibi imetekeleza majukumu mbalimbali ambayo ni:-

- i. *Ukaguzi wa maeneo yanayojihusisha na biashara ya Dawa za Binadamu na Mifugo Vifaa Tiba, Vitendanishi na Maabara.*
- ii. *Usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara ya dawa, vifaatiba na bidhaa nyongeza.*
- iii. *Udhhibit wa uingizaji na usafirishaji wa bidhaa ndani na nje ya nchi.*
- iv. *Ufuatiliaji wa ubora wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika soko.*
- v. *Ufuatiliaji wa usalama na matukio yanayohusiana na matumizi ya dawa*
- vi. *Uteketezaji wa bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora na usalama.*
- vii. *Uchunguzi wa awali wa sampuli za dawa kupitia maabara hamishika.*
- viii. *Kuimarisha utoaji Elimu kwa Umma na kuboresha huduma kwa wateja.*
- ix. *Usimamizi wa mifumo na vihatarishi.*
- x. *Ufuatiliaji wa majukumu ya TMDA yaliyo kasimiwa kwa Halmashauri.*



Bw. Christopher O. Migoha
Meneja wa TMDA, Kanda ya Magharibi

Nachukua nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Kanda ya Magharibi kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuwaomba wazidi kuwa na morali na moyo wa kazi, Vilevile natoa shukrani za dhati kwa Menejimenti ya TMDA kwa maelekezo yao kipindi chote cha kuanzia mwezi Julai 2021 hadi Juni, 2022.



Meneja TMDA Kanda ya Magharibi, Bw. Christopher O. Migoha akitoa ufanuzi kwa vyombo vya habari juu ya dawa zilizo kamatwa.

UKAGUZI WA MAENEKO YANAYOJIHUSISHA NA BIDHAA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2021 HADI JUNI 2022.

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022, Ofisi ya Kanda ya Magharibi imefanya jumla ya kagazi 788 katika Maduka ya dawa za binadamu na mifugo, vifaa tiba, hospitali, vituo vya afya, zahanati na maabara. Na kubaini mapungufu mbalimbali na hatua stahiki za kiudhibiti zilichukuliwa.

Katika kagazi hizoz Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Magharibi imefanikiwa kumkamata mfanyakishara, Zakayo Bagomwa mkazi wa Ulyankulu wilayani Kaliua mkoani Tabora anayemiliki Duka la Dawa za binadamu, liitwalo MALIZA NA YESU kwa tuhuma za kuuza

Dawa za wizi na zilizopigwa marufuku na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zenyet thamani ya shilingi milioni 15,178,400/=.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari Meneja wa TMDA Kanda ya Magharibi, Christopher Migoha amesema mtuhumiwa amekamatwa hivi karibuni na maofisa wa mamlaka hiyo baada ya kupata taarifa za siri na kwenda kufanya ukagazi wa kina katika duka lake na kubaini uwepo wa dawa hizoz zinazouzwa kinyume na sheria.

Aidha, Migoha amesema mtuhumiwa alikutwa akiuza dawa za kifua kikuu (TB), kadi za kliniki za

kina mama wajawazito, kutoa huduma za matibabu ndani ya duka, kuuza vifaa tiba ambavyo ni mali ya Serikali ya Jamhuru ya Muungano wa Tanzania na dawa kutoka Kenya ambazo hazipaswi kuuzwa nchini ikiwemo dawa zinazotolewa bure na serikali kwa wagonjwa.




Baadhi ya dawa za kutibu mifugo zilizokamatwa na Wakaguzi wa TMDA Kanda ya Magharibi

Vingine ni dawa na vitendanishi vya kupimia virusi vya ukimwi na malaria ambavyo ni mali ya serikali ya tanzania vikiwa vimehifadhiwa na kutunzwa kwa ajili ya kuuzwa kinyume cha kifungu cha 312(1) cha kanuni ya Adhabu, Sura 16, dawa zisizosajiliwa kutumika nchini zikiwa zimehifadhiwa na kuuzwa kinyume cha Sheria ya Dawa na Vifaa tiba, Sura 219 pamoja na dawa zisizoruhusiwa kuuzwa katika maduka ya dawa muhimu kinyume na Kanuni ya 63 ya Makundi ya Dawa ya mwaka 2015.

Vilevile Meneja alibainisha katika kaguzi hizo maafisa wa TMDA walikuta dawa zilizokwisha muda wake wa matumizi zikiwa zimetunzwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kuuzwa kinyume na kifungu cha 75(1) cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219, vifaa tiba vya kufanya tohara vikiwa vimetunzwa katika maduka kinyume cha sheria ambavyo havistahili kuwepo wala kuuzwa kwenye maduka ya dawa muhimu.

Mwisho Meneja alitoa wito kwa wafanyabiashara wote wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi kufanya biashara zao kwa kuzingatia Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219 pamoja na Sheria zingine zilizowekwa, kinyume na hapo TMDA haitawavumilia wale wote watakaokiuka Sheria hizo.



UDHIBITI WA UINGIZAJI WA BIDHAA NCHINI.

Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi juni 2022, Ofisi ya Kanda ya Magharibi imetoa jumla ya vibali 6 vya uingizaji wa bidhaa za dawa za binadamu na mifugo Nchini, Huku ikishiriki katika vikao vya pamoja baina ya Taasisi za Serikali ya Tanzania, Serikali ya Burundi na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa ajili ya kuitisha michoro ya ujenzi wa Kituo cha pamoja cha mpakani (One Stop Border Point, OSBP) kitakachojengwa eneo la Manyovu.



Muonekano wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Karema iliyopo Mkoani Katavi.



UFUATILIAJI WA MADHARA YA DAWA, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI.

Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Juni 2022 Ofisi ya Kanda ya Magharibi ilifanya ufuatiliaji katika Vituo vya kutolea huduma za chanjo ya UVIKO-19 vilivyopo Mikoa ya Katavi, Kigoma na Tabora.

Katika ufuatiliaji huo jumla ya watu 1,492 walifanyiwa ufuatiliaji kwa njia ya simu baada ya kupatiwa chanjo ya UVIKO-19 ambapo watu 460 waliripotiwa kupata maudhi madogo madogo baada ya kupatiwa chanjo ya UVIKO-19.

Vilevile katika kipindi hiki cha kuanzia Julai 2021 jumla ya Watumishi wa Afya 68 walihamasishwa juu ya utoaji wa taarifa za madhara yanayoripotiwa baada ya matumizi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi.



*Mkaguzi wa TMDA Kanda ya Magharibi **Bw. Kiboko Magigi** akitoa mafunzo kwa watoa huduma za Afya katika kituo cha Afya cha Nanga, wilayani Igunga juu ya utambuzi na ujazaji wa taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya Dawa, Chanjo na Vifaa tiba.*



ELIMU KWA UMMA



Meneja wa Kanda **Bw. Christopher Migoha** pamoja na mkaguzi **Bw. Fredrick Luyangi** wakitoa elimu kwa umma kuititia kituo cha radio cha Mpanda FM.

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba TMDA Kanda ya Magharibi imeendesha zoezi la utoaji wa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya dawa, vifaa tiba, vitendanishi na viuavijasumu vikienda sambamba na kuwafahamisha wananchi kuhusu majukumu na wajibu wa TMDA katika udhibiti wa tumbaku na bidhaa zitokanazo na Tumbaku.

Katika kuhakikisha elimu inawafikia wananchi wa kanda hiyo TMDA imetoa elimu kuititia vyombo vya habari, Vikao na wadau, wafanyabiashara na wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo vilivyopo Kanda ya Magharibi ambapo jumla ya wanafunzi 22,402 na waalimu 748 wamefikiwa.



Mkaguzi wa Kanda ya Magharibi **Bw. Fredrick Luyangi** akitoa maelezo kuhusu matumizi sahihi ya dawa katika programu ya elimu kwa umma iliyofanyika katika shule ya sekondari ya wasichana ya Kibondo.



Mkaguzi wa Kanda ya Magharibi **Bw. Fredrick Luyangi** (Hayupo pichani) akitoa maelezo kuhusu matumizi sahihi ya dawa katika programu ya elimu kwa umma iliyofanyika katika shule ya sekondari ya Misunkumilo ilipo mkoani Katavi.



Meneja wa Kanda ya Magharibi **Bw. Christopher Migoha** akitoa maelezo kuhusu udhibiti wa tumbaku katika kikao na wadau pamoja na wafanyabiashara kilichofanyika tarehe 25 Juni, 2022 mkoani Tabora.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora **Bw. Msalika Makungu** akifungua kikao kazi cha wadau wa tumbaku na wafanyabiashara wa Mkoa wa Tabora.



Mkaguzi wa dawa wa Kanda ya Magharibi **Bw. Fredrick Luyangi** akijibu maswali kutoka kwa wadau wa tumbaku katika kikao cha kutambulisha jukumu jipya la udhibiti wa tumbaku pamoja na Sheria zinazoongoza utekelezaji wa jukumu hilo mkoani Katavi.



Meneja wa Kanda **Bw. Christopher Migoha** akitoa elimu kwa wanafunzi wa shule ya sekondari ya Rungwa mkoani Katavi.



TMDA KUSHIRIKI KONGAMANO LA KIMATAIFA

Katika kufikisha elimu kwa jamii Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba nchini TMDA Kanda ya Magharibi imeshiriki katika kongamano la kimataifa na maonesho ya biashara ya nchi zilizo jirani na Ziwa Tanganyika, ili kutoa elimu juu ya majukumu ya mamlaka hiyo.

Maonyesho hayo yaliyofanyika mkoani Kigoma na kushirikisha nchi za Burundi, Congo DRC, Rwanda, Zambia na Tanzania iliyokua mwenyeji yalibeba kauli mbiu ya "**Mipaka yetu kukuza uwekezaji na Biashara**", yalifunguliwa na waziri wa TAMISEMI **Mh. Innocent Bashungwa** aliye kua mgeni rasmi na watu zaidi ya 276 walitembelea banda la TMDA.

Mbali na TMDA Taasisi mbalimbali na wafanyabiashara kutoka katika nchi hizo waliweza kuonesha kazi zao na kutangaza fursa mbalimbali za kibashara ambazo zinaweza kuvuka mipaka ya Nchi moja kwenda Nchi nyingine na hivyo kukuza uwekezaji na kupata faida pamoja na kudumisha Amani na mahusiano mema baina ya Nchi hizi.



*Waziri wa Tamisemi **Mh. Innocent Bashungwa** akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Kanda ya Magharibi juu ya majukumu ya TMDA katika Kongamano la Kimataifa na maonesho ya Biashara ya nchi zilizo jirani na Ziwa Tanganyika.*



MARUFUKU YA MATUMIZI YA BIDHAA ZA TUMBAKU.

Meneja (TMDA) Kanda ya Magharibi **Bw. Christopher Migoha** amepiga marufuku matumizi ya bidhaa za tumbaku katika maeneo yote yenye mkusanyiko wa watu ili kuendelea kuilinda Afya ya jamii ambayo haitumii bidhaa hizo.

Bw. Migoha ametoa katazo hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juu ya madhara ya bidhaa zitokanazo na mazao ya tumbaku ambapo ameeleza bidhaa ambazo hazitakiwi kutumiwa maeneo yenye mkusanyiko wa watu ni pamoja na sigara, siga, sigarusi, misokoto, shisha, kiko, tumbaku ya unga na bidhaa nyingine zinazo fanana na hizo.

Aidha, Migoha Aliyataja maeneo hayo yenye mikusanyiko ya watu ni yale yanayotoa huduma za Afya, Maktaba, mahali pa Ibada, majengo au maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mikutano ya kitamaduni na kijamii, shughuli za michezo na burudani, kumbi za starehe, Usafiri wa Umma, na ofisini.



Maeneo mengine aliyoyataja ni sehemu za huduma ya chakula, vyombo vya usafiri wa anga, ardhi, maji, mabanda ya maonesho, masoko / magilio, maduka makubwa na maeneo mengine yoyote yanayotumiwa na Umma.

Migoha alifafanua kuwa sheria imeruhusu uvutaji wa bidhaa za tumbaku kwenye maeneo ya taasisi za elimu ya juu, majengo ya ofisi, hoteli, baa, migahawa na maeneo ya burudani ambayo yanatakiwa kuwa yametenga vyumba maalumu ya kuvutia bidhaa hizo, huku akiwataka wananchi wote wa Tabora kuzingatia utekelezaji wa Sheria hiyo ambayo imetakiwa kuanza mara moja maeneo yote ya Umma.

UTEKETEZAJI WA DAWA

TMDA Kanda ya Magharibi imeteketeza jumla ya kilo 51820 ya bidhaa za dawa na vifaa tiba zinazokiuka Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 zenye thamani ya shilingi 2,672,233,477/= . Bidhaa hizi zilipatikana baada ya kagazi mbalimbali na zile zilizopokelewa baada ya wamiliki kutuma maombi ya uteketezaji wa hiari.



Kichomea taka (Incinerator) inayotumika kuteketeza bidhaa zinazodhibitiwa na TMDA Kanda ya Magharibi, kilichopo katika Hospitali ya St. GASPAR, Singida.

HUDUMA KWA JAMII



Meneja wa TMDA Kanda ya Magharibi **Bw. Christopher Migoha** akikabidhi dawa zinazofaa kwa matumizi kwa Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Dawa hizi ni zile zilizoondolewa maeneo mbalimbali katika Kanda ya Magharibi kufuatia wamiliki kukiuka kanuni ya 63 ya makundi ya dawa ya mwaka 2015.



Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

**MAMLAKA YA DAWA
NA VIFAA TIBA**

*Kanda ya Magharibi,
Jengo la NSSF,
Mtaa wa Jamhuri,
S.L.P 520, Tabora
Simu +255 262606082
Barua pepe: info.tabora@tmda.go.tz*

